# Tafsiri za Fasihi ya Kiswahili na Mchakato wa Utandawazi

*Clara Momanyi*

**Ikisiri**

Katika muktadha wa ubadilishanaji wa maarifa, ujuzi na sayansi, utandawazi si dhana ngeni. Hii ni kwa sababu ubadilishanaji huu miongoni mwa nchi mbalimbali uliwezeshwa na mchakato wa utandawazi mkongwe uliokita mizizi hususan katika karne za 16 hadi 19. Tamaduni nyingi ulimwenguni zimeweza kupiga hatua za kimaendeleo kutokana na ubadilishanaji wa habari na maarifa kwa njia ya tafsiri. Sanaa za uandishi miongoni mwa jamii mbalimbali za ulimwengu zimepokezwa kwa muda mrefu kupitia tafsiri. Mchepuo wa lugha na taaluma za tafsiri vilichangia na vinaendelea kuchangia kasi ya utandawazi huo na hivyo, kuzijenga na kuziimarisha tafsiri za fasihi mbalimbali ulimwenguni. Kutokana na uhalisi huu basi, makala yanaldurusu suala la tafsiri za kifasihi hususan katika muktadha huu wa utandawazi. Aidha, yanajadili umuhimu wa tafsiri za matini za fasihi ya Kiswahili katika mawanda ya utandawazi kwa kuzingatia faida zake katika kueneza utamaduni, falsafa na maadili yetu.

## 1.0 Utangulizi

Tamaduni nyingi ulimwenguni zimeweza kupiga hatua za kimaendeleo kutokana na ubadilishanaji wa maarifa miongoni mwa jamii mbalimbali. Njia mojawapo ya kufaulisha hali hii ni kupitia ufasiri au utafsiri. Kwa mfano, Kelly (1979:1) anaeleza kwamba Ulaya Magharibi ilifaidi ustaarabu na maendeleo kutokana na juhudi za mfasiri. Kufaulu kwa Himaya ya Roma hadi kufikia ustawi wa taaluma za kimataifa katika mambo ya biashara na utawala kulifanikishwa na taaluma ya tafsiri. Utamaduni wa Kirumi uliathiriwa na ule wa Kiyunani kupitia tafsiri. Aidha, inakisiwa kwamba Pythagoras hakuasisi ule uhakiki wake wa kimantiki hadi alipozuru Afrika. Wamisri walikuwa na utaalamu wa hisabati, unajimu na sayansi kabla hata ya nyakati za Pythagoras. Hata Plato alizuru Misri, barani Afrika ili kupata maarifa ya kifalsafa. Bila shaka uelewa wa watu hawa ulichangiwa zaidi na tafsiri.

Hadi kwenye karne ya 19, utamaduni wa Ulaya ulikuwa umeathiriwa sana na tafsiri za lugha za Kiyunani na Kilatini. Nao utamaduni wa Kijerumani uliweza kuathiriwa kwa kiasi na fasihi ya William Shakespeare wa Uingereza. Kwenye karne hiyo ya 19, tamaduni nyingi za Kiafrika ziliathiriwa na tamaduni za Ulaya hasa kupitia tafsiri za kifasihi kutoka katika lugha za kimagharibi kwenda katika lugha za Kiafrika, ikiwemo lugha ya Kiswahili. Kihistoria, Ugiriki je, mbona hawa hawajulikani kabisa? Sababu mojawapo ni kwamba Wagiriki kama vile Hegel (1770-1831) walifanya juhudi za kufutilia mbali kabisa historia ya Afrika pamoja na habari zote kuhusu bara hili kwani waliamini kwamba Afrika sio sehemu ya historia!

Tukirejelea mawanda ya fasihi barani Afrika ni kwamba tuna machimbo mengi ya fasihi zetu, hususan hadithi za kale kutoka katika jamii mbalimbali. Baadhi ya hadithi hizi zilipokezwa kwa njia ya mdomo kupitia tafsiri, kukiwemo pia matukio ya kale

yaliyosisimua jamii. Je, tunafahamu kwamba zile hadithi za Esopo zilizotafsiriwa zilitungwa na Mhabeshi aliyepelekwa katika nchi za Ulaya kama mtumwa? Leo hii tunazipokea kupitia tafsiri. Hii ni kupitia utafiti wangu mkoani pwani nchini Kenya (tarehe 16-20 Mei 2012). Tufahamu pia kwamba kuanzishwa kwa maingiliano baina ya mataifa mbalimbali kupitia kwa nguvu za utandawazi kumekutanisha pia lugha na tamaduni za mataifa hayo. Hali hii pia huchangia ubadilishanaji wa tanzu za kifasihi na hivyo basi kuelewa kaida za maisha na tamaduni za watu mbalimbali ulimwenguni. Katika dahari hizi, tafsiri nyingi za maandishi ya kifasihi kutoka katika mataifa mbalimbali ya ulimwengu zinatufikia barani Afrika ama kupitia lugha za kikoloni au kupitia lugha zetu asilia. Hivi leo, Kiswahili kina dafina kubwa ya fasihi tafsiri za ulimwengu. Lakini hii haitoshi. Tunahitaji kuwa na hazina kubwa zaidi ya tafsiri za kifasihi katika lugha ya Kiswahili ili ubadilishanaji wa maarifa, falsafa na utamaduni viweze kukita zaidi katika nyakati hizi za utandawazi. Fasihi ya Kiswahili pia haina budi kutafsiriwa kwa mapana zaidi katika lugha za kigeni ili kuusambaza utamaduni wetu pamoja na lugha ya Kiswahili kama lugha ya kimataifa.

## 2.0 Dhana ya Tafsiri

Dhana ya tafsiri imetolewa maana mbalimbali kwa lengo la kuielewa. Kulingana na Mwansoko (2006:1), tafsiri ni zoezi la uhawilishaji wa mawazo katika maandishi kutoka lugha moja hadi nyingine. Aidha, anasema kwamba tafsiri ndilo daraja linalounganisha jamii mbalimbali za watu wanaotumia lugha zinazotofautiana. Kadhalika, ni wenzo wa kueneza utamaduni, falsafa, maarifa na fasihi kutoka jamii moja hadi nyingine. Nakubaliana kabisa na mawazo haya kwani wanadamu huweza kuingiliana na wengine katika maeneo mbalimbali ulimwenguni kwa kiasi kikubwa wakiwezeshwa na tafsiri za lugha. Kwa upande wake, Catford (1965:20) anasema kuwa kufasiri ni kuchukua mawazo yaliyo katika maandishi kutoka lugha chanzi na badala yake kuweka mawazo yanayolingana katika lugha lengwa. Akifafanua dhana ya tafsiri, Omboga (1986) anaeleza kwamba mfasiri hana budi kuwa na ujuzi wa lugha chanzi na lugha lengwa au pokezi, hasa utamaduni wa lugha hizo, isimu, sarufi na ujuzi wa kitaaluma kuhusu matini anayotafsiri. Hapa basi, ulinganifu wa mawazo, utamaduni na vipengele vya lugha ndiyo mambo muhimu ya kuzingatiwa katika tafsiri za kifasihi. Tunakubaliana na Omboga kwani mfasiri hana budi kuufahamu barabara utamaduni wa lugha chanzi, mbali na kuwa mweledi katika kuitumia lugha hiyo katika miktadha inayokubalika katika jamii. Hili humwezesha kuitafsiri matini ya kifasihi bila kupotosha maana iliyokusudiwa na mwandishi wa zao hilo.

Hata hivyo, tuelewe kwamba kuna mitazamo mingi inayozungumzia yale yaliyo muhimu katika kutafsiri. Kama anavyoeleza Newmark (1988:19), nadharia ya tafsiri si nadharia wala sayansi, bali ni mfumo wa ujuzi tulio nao na tunaopaswa kuwa nao kuhusu michakato ya kutafsiri. Hivyo basi tunaweza kusema pia kwamba nadharia za tafsiri zinaweza kutumika kwa kutegemeana ili ziweze kurutubisha tafsiri. Hii inatokana na ujuzi au weledi alio nao mfasiri katika kuteua vigezo vinavyofaa na kwa

kutegemea matini tofauti tofauti. Tukirejelea utaalamu wa kutafsiri kazi za kifasihi, tunaweza kutoa kauli kwamba matini za kifasihi ni ngumu au hutatiza kutafsiri. Hali hii hufanywa ngumu zaidi kwa sababu matini hizo huandikwa kwa lugha ya kisanaa, kwa hivyo mfasiri hana budi kutumia ujuzi mkubwa ili kunasa maana iliyokusudiwa. Anawajibika kupigia mbizi miundo ya kisanii iliyotumiwa, zikiwemo zana za kitamathali, pamwe na vivuli vya maana za kitamaduni vinavyoweza kumfikirisha zaidi. Kwa hivyo hapa tunaweza kukubaliana na Mwansoko katika *Kitangulizi cha Tafsiri* (2006:42) kwamba ufasiri wa kifasihi ni tukio la sanaa na sio la isimu. Changamoto zingine zinazoweza kumsumbua mfasiri wa aina hii pia ni pamoja na tofauti za kiisimu, kiitikadi, kihistoria na kimazingira zilizoko katika lugha chanzi na lugha lengwa. Changamoto hizi huweza hata kusababisha mfasiri au mfasiri kubadili maana iliyokusudiwa na mwandishi asilia. Ijapokuwa utandawazi umeufanya ulimwengu kuwa mfano wa kijiji, bado kuna tofauti za kimaisha miongoni mwa jamii mbalimbali ambazo lazima zizingatiwe pale tunapofanya tafsiri za matini za kifasihi. Tukirejelea tafsiri za kifasihi, Mtesigwa katika *Kitangulizi cha Tafsiri* (2006:88) anafafanua kwamba mfasiri wa matini za kifasihi hana budi kuwa mahiri wa lugha zote mbili anazoshughulikia, hususan miundo yake na matumizi kulingana na tamaduni zinazohusika. Aidha, atahitajika kuifahamu vyema mada anayotaka kuifasiri na hapaswi kuongeza au kupunguza chochote cha mwandishi asilia. Hana budi pia kumfahamu vyema mwandishi wa matini chanzi, hasa kujua dhamira yake na kile kilichomchochea kuandika aliyoandika na kwa namna alivyoandika. Haya yatachangia katika kuielewesha hadhira lengwa kuhusu kisa chenyewe na vivyo hivyo kuupata uhondo wa kisanaa aliokusudia mwandishi asilia. Hivyo basi, tafsiri nzuri ni ile inayojumuisha na kuhifadhi uasili wa kazi asilia.

Katika kuangazia tafsiri za kifasihi pia, Snell-Hornby (2006:21) akimnukuu Jakobson (1959) anaeleza kwamba utanzu wa ushairi ndio mgumu zaidi kutafsiri kutoka lugha chanzi hadi lugha pokezi. Kuna changamoto nyingi ambazo mfasiri huweza kukumbana nazo hasa kwa kuzingatia vipengele vya umbo, muundo na maudhui. Haya huzua utata wa kupatikana kwa maana inayolengwa na mshairi. Hivyo, Jakobson aliishia kusema kwamba ushairi hauwezi kutafsiriwa. Hata hivyo, kutokana na mabadiliko ya kielimu na kisayansi katika jamii, utanzu huu umeweza kutafsiriwa hasa katika maeneo ya Afrika Mashariki ambapo tenzi za kale za Kiswahili zilizoandikwa kwa kutumia hati za Kiarabu zimeweza kufasiriwa na maana kubainika wazi bila tashwishi yoyote. Sio lengo la makala haya kujadili nadharia mbalimbali za tafsiri, maoni mbalimbali ya watu kuhusu suala zima la tafsiri, mapungufu wala faida zake. Mada yetu kuu inajadili umuhimu wa tafsiri za kifasihi, hususan kwa kuzingatia zile za fasihi ya Kiswahili katika mchakato wa utandawazi.

### 3.0 Tafsiri katika Mawanda ya Fasihi ya Kiswahili na Utandawazi

Lugha ya Kiswahili imetumiwa kufasiria masuala mbalimbali ya kijamii katika jamii zetu hasa katika nyanja za elimu na maisha ya jamii. Hata hivyo, taaluma hii ina upungufu mkubwa inapokuja katika masuala ya kutafsiri fasihi ya Kiswahili kwenda katika lugha zingine za kimataifa. Barani Afrika, utandawazi umehusishwa na mchapuko wa mawasiliano mapana, biashara huria, mbali na masharti magumu ya kibiashara yanayolenga kunufaisha mataifa tajiri. Baadhi ya hoja zinazotolewa na watu mbalimbali ni kwamba utandawazi umechangia katika kuhalalisha umaskini barani Afrika. Hali kadhalika, dhana ya utandawazi inahusisha matumizi ya lugha za kimataifa kama vile Kiingereza, Kifaransa na Kijerumani, lugha zinazosambaza ajenda za kimataifa na ukiritimba wa mataifa tajiri. Lakini kwa mataifa yanayoendelea, huu sio wakati wa kulalama au kukashifu kwani tayari mchapuko huo wa utandawazi mpya sasa ni kama sehemu ya maisha ya kila siku katika jamii nyingi ulimwenguni. Jamii nyingi barani Afrika hazikusazwa na mabadiliko haya ya utandawazi na teknolojia pevu za mawasiliano. Ni juu ya Waafrika sasa kuyavulia nguo maji na kuyaoga. Sio wakati wa kuwa watazamaji bali wakati wa kujitosa kwenye kinyang'anyiro hiki ili wao pia watambulike kupitia usambazaji wa maarifa, falsafa, maadili na fasihi katika medani za kimataifa.

Hivyo basi, wenyeji wa Afrika Mashariki wanaotumia Kiswahili, hususan wanafasihi hawana budi kutafsiri fasihi zilizo katika tanzu mbalimbali kutoka katika lugha chanzi ya Kiswahili na kwenda katika lugha lengwa mbalimbali. Wasingojee wasomi wa fasihi kutoka katika mataifa ya kigeni kutoa tafsiri za fasihi ya Kiswahili kwa lugha zao bali wawe katika mstari wa mbele kuzifanyia kazi zao wenyewe tafsiri. Aidha, fasihi za kiasili kama vile tenzi, hadithi na michezo ya kuigiza kutoka katika lugha mbalimbali asilia zinahitaji kutafsiriwa kwa Kiswahili kama alivyofanya Aniceti Kitereza aliyefasiri riwaya yake iitwayo *Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka Ntulanwalo na Bulihwali* (1980) kutoka lugha chanzi ya Kikerewe hadi Kiswahili (Mwansoko, 2006:6). Riwaya hii pia inaweza kutafsiriwa kwa Kiingereza au lugha lengwa nyingine yoyote. Hivi ndivyo Afrika Mashariki, kwa mfano, inavyoweza kukuza fasihi zake kimataifa.

Katika eneo la Afrika Mashariki, historia inatuonesha kwamba harakati za kufasiri kazi za fasihi zilikuwa zikifanyika tangu karne ya 18. Baadhi ya wahakiki wa fasihi ya Kiswahili kama vile Knappert (1979) wameeleza kwamba tafsiri maandishi katika fasihi ya Kiswahili ilianza mwaka wa 1749 wakati ambapo ule utenzi wa Kiarabu uliojulikana kama *Umm-ul Qura* ulitafsiriwa kwa Kiswahili na Aidarus bin Athman na kujulikana kama *Utenzi wa Hamziyya*. Karne za 19 na 20 nazo zilishuhudia ufasiri wa kazi nyingi za fasihi za kigeni kwa lugha ya Kiswahili kama vile *Hekaya za Abunwasi na Hadithi Nyingine*, *Alfu-Lela-Ulela* (siku elfu na moja), *Hadithi za Esopo*, *Safari za Guliva*, *Robinson Kruso na Kisiwa chake* na *Elisi katika Nchi ya Ajabu*, miongoni mwa zingine. Baada ya uhuru katika nchi za Afrika Mashariki pia

zikatolewa tafsiri za vitabu vya William Shakespeare kama vile *Juliasi Kaizari* na *Mabepari wa Venisi*, kazi zilizotafsiriwa na Mwalimu Julius Nyerere (1969). Aidha, *Wimbo wa Lawino* ni tafsiri iliyotolewa na Paul Sozigwa, miongoni mwa tafsiri zingine. Katika nchi hizi hivi sasa hakuna taasisi yoyote ya Afrika Mashariki inayoshughulikia taaluma ya tafsiri isipokuwa nchini Tanzania ambapo Baraza la Kiswahili Tanzani (BAKITA) lilianzishwa mwaka 1967 ambalo lina Idara ya Tafsiri, na Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI) ikaanzisha kitengo cha Istilahi na Tafsiri ili kutoa huduma za ufasiri mwaka 1986. Juhudi zinazofanywa na vyombo hivi hazishirikishi nchi zile zingine za Afrika Mashariki. Kutokana na ukosefu wa ushirikiano huu, tafsiri na istilahi huundwa kipekee katika nchi hizi na hakuna uwiano kamili unaojitokeza. Hili ni suala linalohitaji kushughulikiwa kwa haraka iwapo wenyeji wa janibu hizi wanataka lugha ya hii iweze kupiga hatua za kimataifa.

Baadhi ya wataalamu wa tafsiri pia wamebainisha mambo kadhaa yanayoweza kumtatiza mfasiri wa matini hasa za kifasihi. Changamoto hizi ni kama vile dhana au istilahi za kifasihi zinazoibuliwa kwa kasi kwa kadri ambavyo mchepuo wa utandawazi unazidi kupiga kambi katika janibu za Afrika Mashariki. Aidha, kuingizwa maneno mapya kwa kasi katika Kiswahili kunakosababishwa na maendeleo ya kisayansi na kiteknolojia huchangia utata wa tafsiri, hususan kutoka lugha za kigeni hadi Kiswahili au hata kutoka lugha chanzi ya Kiswahili kwenda katika lugha lengwa. Kwa mfano, Watanzania huridhika kutumia neno 'Kompyuta' kuliko 'Tarakilishi' linalotumika nchini Kenya kwa dhana ya 'Computer'. Au pia katika kunyambua maana ya 'Feminism' ambayo nchini Tanzania inakuwa 'Ufeministi' na nchini Kenya aghalabu neno 'Unisai' hutumiwa. Kadhalika, 'Sexism' ni dhana iliyoingizwa katika mazingira ya eneo la Afrika Mashariki kutokana na mchakato wa utandawazi na harakati za masuala ya kike au haki za binadamu. Je, tunaweza vipi kubainisha tofauti baina ya 'Gender' na 'Sexism'? Aghalabu maneno 'Ujinsia/Jinsia' hutumiwa ili kuchukua maana ya dhana zote mbili ilhali tunajua kuwa kuna tofauti kimatumizi. Je, dhana ya 'Gender' tuiite 'Umenke' au 'Uana'? Maneno haya yanatokana na mijadala inayozuka nchini Kenya katika mihadhara na makongamano ili kutafuta istilahi muafaka zinazoweza kubeba uhalisi wa dhana hizo. Haya ni baadhi ya masuala ambayo yanaweza kumshughulisha mfasiri anapoingia katika mawanda ya kutafsiri matini za kifasihi hususan katika uchambuzi wa kinadharia.

Tunapotafsiri matini za kifasihi zilizoasisiwa Uingereza, kwa mfano, tunaweza kukumbana na pingamizi mbalimbali kama vile desturi za malaji yao ambayo hayapo katika utamaduni za Afrika Mashariki. Kwa mfano, Mwansoko katika *Kitangulizi cha Tafsiri* (2006:33-34) anatoa mfano mahususi wa vyakula kama vile breakfast, high tea, lunch, dinner au supper. Tunapojaribu kutafsiri maneno haya kwa Kiswahili hasa yanapojitokeza katika matini chanzi zilizoandikwa kwa Kiingereza huenda tukapata

matatizo. Haya ni baadhi tu ya matatizo yanayoweza kumkabili mfasiri kutokana na ile hali kwamba tamaduni na desturi za kigeni ni tofauti na za maeneo haya. Kadhalika, tunapojaribu kutafsiri fasihi za Afrika Mashariki zilizoandikwa kwa lugha ya Kiswahili hadi kwa lugha lengwa za kigeni, huenda pia tukakumbwa na matatizo yanayotokana na tamaduni au desturi za janibu hizi ambazo hazina uwiano na zile za ughaibuni. Tuelewe pia kwamba kutafsiri ni mchakato unaohusu utamaduni. Hivyo basi, katika fasihi msamiati una nafasi kubwa ya kujenga maana kutokana na utamaduni wa jamii inamozungumziwa lugha hiyo. Utafsiri wa matini za kifasihi hauna budi kujishughulisha na maana fiche za kitamaduni zilizoko kwenye matini chanzi ili zao hilo la tafsiri liweze kueleweka katika muktadha uliokusudiwa na mwandishi asilia. Ijapokuwa Temu (1972:1), kwa mfano, anasema kwamba Kiswahili kinaweza kuzalisha istilahi zote zinazohitaji kueleza chochote katika nyanja zote za taaluma, lazima istilahi hizo pia ziafiki miktadha ya kimatumizi na vizio vya maana vinavyohusishwa pale ambapo tafsiri za kifasihi zinahusika.

Kwenye mwaka wa 2001, Umoja wa Nchi za Afrika ulianzisha Taasisi iitwayo ACALAN ili kusawazisha na kuendeleza lugha za Kiafrika. Inasikitisha kuona kwamba ujenzi wa mikakati ya kutafsiri shehena kubwa ya fasihi za lugha hizi haupo na kama upo, unadorora na hatuusikii. Bara la Afrika linakisiwa kuwa na takriban lugha 2000. Bila shaka lugha hizi zimebeba mgodi mkubwa wa fasihi unaosubiri kutafsiriwa na kusambazwa kwa mataifa ya nje kupitia kwa lugha za kimataifa zilizo na nafasi kubwa katika mtandao wa mawasiliano. Kwa muda mrefu sasa, serikali za nchi za Afrika Mashariki hazijatilia maanani taaluma ya tafsiri wala ukalimani. Kutokana na kasi ya utandawazi ulimwenguni, kuna soko kubwa la taaluma hizi ambalo linasubiri kufunguliwa kutokana na nafasi ya Kiswahili sasa katika eneo hili na maeneo ya maziwa makuu. Hivyo, kasi ya TEHAMA (Teknolojia ya Habari na Mawasiliano) ijibiwe na kasi ya uzalishaji wa wafasiri mbalimbali watakaoweza kufasiri fasihi zetu kwa lugha za kigeni ili kulifungua soko hili. Mafarisi wa kifasihi tunaowanukuu kila uchao kama vile William Shakespeare wa Uingereza na mshairi msifika Abu Nuwas (756-810) wa Arabuni ni matokeo ya tafsiri. Kiswahili kimetumiwa kutafsiri fasihi za ughaibuni kwa kiasi kikubwa lakini jambo la kusikitisha ni kwamba shehena yake ya kifasihi haitafsiriwi kwa lugha zingine.

Aghalabu hatuwatambui ipasavyo magwiji wa fasihi ya Kiswahili kama vile Said Khamis Mohammed, Euphrase Kezilahabi, Adam Shafi, Wadi Wamitila na wengineo. Badala yake tunasoma magazetini kila uchao hasa nchini Kenya tahakiki za waandishi walioandika kazi zao kwa lugha ya Kiingereza juu ya wanafasihi kama vile Francis Imbuga, Ngugi wa Thiong'o, David Maillu na wengineo. Wahakiki wengine nchini Kenya hata wametoa kauli muflisi kuwa fasihi ya Kiswahili imesalia kuwa jangwa lenye ukame kwani waandishi hawapo. Hii si kweli kwa sababu wanafasihi wa Kiswahili wako wengi. Tatizo ni kwamba hawasikiki kwa sababu huandika kwa Kiswahili, lugha ambayo haifahamiki miongoni mwa wasomi wengi nchini Kenya.

Hali hii pia huenda imechangiwa na ukosefu wa tafsiri za vitabu vya fasihi ya Kiswahili kwa lugha zingine kama vile Kifaransa, Kiingereza, Kijerumani au hata Kihispania. Hili ndilo jukumu ambalo hatuna budi kulishughulikia katika nyakati hizi za teknolojia pevu za mawasiliano zinazoweza kurahisisha usambazaji wa fasihi tafsiri kwa mataifa mbalimbali. Hata hivyo, waandishi wa makala mbalimbali wamebainisha kuwa zipo baadhi ya kazi za fasihi ya Kiswahili ambazo tayari zimeshatafsiriwa kwa lugha za kigeni.

Kwa mfano, Aiello (2005) akimnukuu Bertoncini-Zubkova (2004), anaeleza kwamba wapo wanafunzi wa Kiitaliano ambao tayari wametafsiri kazi mbalimbali za fasihi ya Kiswahili katika tafiti zao. Baadhi yao wananuia kuchapisha kazi hizo kwa lugha ya Kiitaliano. Bila shaka huu utakuwa mchango mkubwa katika hazina ya fasihi tafsiri ya Kiswahili. Hatua hii itachangia kueneza fasihi za Afrika Mashariki sio tu barani Ulaya bali pia katika mataifa mengine ulimwenguni. Uakibishaji na usambazaji wa fasihi kupitia kwa mtandao wa mawasiliano ulimwenguni ni njia moja ya kuiwezesha fasihi ya aina hii kusafirishwa na kupokewa kwa kazi zaidi. Akigusia suala la tafsiri pia, Aiello (2005: 103) anaeleza kwamba kutafsiri kazi bunifu za Kiswahili kwa Kiitaliano kutafungua ukurasa mpya wa kupata wasomaji zaidi wa kazi hizo. Hivyo basi, kuchapisha fasihi ya Kiswahili iliyotafsiriwa kwa Kiitaliano au kusomwa katika nyavuti mbalimbali za mitandao ya mawasiliano kutaondoa lile pengo la ukosefu wa tahakiki za fasihi tafsiri za Kiswahili nchini Italia. Ili kushadidia umuhimu wa kutafsiri fasihi ya Kiswahili na kusomwa na mataifa mengine, Aiello ametafsiri riwaya ya S.A. Mohamed *Utengano* (1980) kwa Kiitaliano na ambayo ilichapishwa mwaka 2005 na kuitwa *Separazione* (Aiello, 2005: 104). Hii ni njia moja ya kusambaza utamaduni wa Kiswahili kwa mataifa ya ulimwengu. Baadhi ya riwaya za Kiswahili pia zimefanyiwa tafsiri kwa lugha za kigeni. Mifano ni kama vile riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad* iliyoandikwa na Shafi Adam Shafi (1978) na ambayo ilitafsiriwa kwa Kifaransa na Karthala na kuchapishwa kwa anuwani *Les gerofliers de Zanzibar* mnamo mwaka 1986. Baadaye riwaya hii ilitafsiriwa upya na Serpent Plumes katika mwaka wa 2000 na kuitwa *Die Sklaverei der Gewurze* (Aiello, 2005:100-101).

Kulingana na Aiello (2005: 101) pia, baadhi ya kazi za mahashumu Shaaban Robert pia zimeshatafsiriwa kwa Kirusi. Chini ya usimamizi wa Andrei Zhukov (1998: 185). Chapisho la kwanza lililotolewa katika mwaka wa 1968 lilihusisha tafsiri za vitabu vya Shaaban Robert kama vile *Kusadikika, Adili na Nduguze, Maisha yangu, Wasifu wa Siti Binti Saad* pamoja na insha zake nyingine. Kusanyiko la kazi hizi linaitwa *Moya zhizn* kwa Kirusi, yaani "Maisha Yangu". Chapisho la pili lilitolewa mwaka 1981 na lilihusisha *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini, Siku ya Watenzi wote, Utubora Mkulima* na *Wasifu wa Siti Binti Saad.* Chapisho hili linaitwa kwa Kirusi *Izbran noye* kumaanisha "Kazi Teule" (Zhukov, 1998:185). Kazi hizi pia

zikiwekwa kwenye mitandao ya mawasiliano zinaweza kusomwa na idadi kubwa ya watu, na hivyo kueneza utamaduni wa watu wa Afrika Mashariki. Hivyo basi mchakato wa utandawazi unaweza kusambaza fasihi tafsiri za ulimwengu kwa kasi zaidi kupitia teknolojia za kisasa za mawasiliano.

Katika mawanda ya teknolojia ya lugha na nafasi yake katika tafsiri, zipo asasi zinazoshughulikia makuzi ya teknolojia ya aina hii, hususan katika muktadha wa lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, Chuo Kikuu cha Helsinki, Ufini, chini ya mradi uitwao 'Swahili Language Manager' (SALAMA), shughuli ya kuunda kanzi data ya Kiswahili inaendelea pamoja na harakati za kutengeneza tafsiri-mashine. Hili litachangia pakubwa juhudi za kutafsiri matini za fasihi ya Kiswahili kwa lugha mbalimbali. Aidha, Kampuni ya *Trans Techno* ya Ufini pia imo katika harakati za utungaji wa kamusi, hususan kusawidi kamusi kamili ya Kiswahili-Kiingereza. Tafsiri ni shughuli ambayo hutegemea pia kamusi za aina mbalimbali ili kuiboresha. Hivyo, mradi huu utasaidia katika tafsiri za matini za kifasihi zilizo katika lugha ya Kiswahili na kwenda katika lugha nyinginezo. Kuna juhudi za kiteknolojia pia za kufanya tafsiri za moja kwa moja kutoka Kiswahili hadi Kiingereza. Bila shaka vyuo na taasisi kama hizi zinatupa mwanya wa matumaini katika kurahisisha mawanda ya tafsiri ili kuzalisha kazi za tafsiri kwa kasi zaidi. Matumizi ya Kiswahili kwenye mtandao wa mawasiliano yanaweza kuzidisha kasi ya uzalishaji na usambazaji wa fasihi tafsiri kwa mataifa mbalimbali. Tufahamu pia kwamba kiasi kikubwa cha istilahi za Kiswahili kinatokana na utohozi wa maneno mengi ya Kiingereza na Kiarabu. Kwa upande mwingine, Kiswahili kama lugha ya kimataifa pia imechangia kimsamiati lugha kama vile Kiingereza. Hivyo basi, taaluma ya tafsiri inaweza kuchangia makuzi ya fasihi tafsiri katika lugha hizi.

**4.0 Hitimisho**

Katika kuhitimisha, lingekuwa jambo bora iwapo kungekuwa na vituo vya ufasiri na ukalimani kote Afrika Mashariki ili taaluma ya tafsiri ipewe aula. Vituo kama hivi vingeweza kujenga ushirikiano wa kitaaluma katika maswala ya tafsiri. Nchini Kenya, kwa mfano, Katiba (2010) mpya imetambua Kiswahili kama mojawapo ya lugha rasmi. Njia mojawapo ya kutekeleza utambuzi huu ni kupitia kutafsiri majuzuu, madaftari na mabuku ya serikali, kukiwemo pia juhudi za kutafsiri fasihi asilia kwa lugha za kigeni ili kusambaza utamaduni wa jamii hii. Ulimwengu unazidi kufinyangwa na kuwa kijiji, hivyo basi jitihada za kutafsiri ziende sambamba na kasi ya utandawazi. Aidha, ipo haja ya kuhakikisha kuwa tuna kanzi ya istilahi za kutosha za kifasihi, pakiwemo makamusi maalumu yanayolenga wakati uliopo ili kufanikisha tafsiri hizo. Kutokana na teknolojia ya mawasiliano, kazi ya tafsiri itakuwa nyepesi. Kinachohitajika ni ushirikiano wa wasomi na wataalamu wa Kiswahili ili kuipigia mbizi shughuli hii. Wanafunzi wanaosomea taaluma za Kiswahili aghalabu hutatizika kutokana na uchache wa vitabu vya kitaaluma vilivyotafsiriwa kwa Kiswahili. Ipo haja ya kupanua marejeleo ya taaluma ya tafsiri kwa lugha ya Kiswahili ili wanafunzi

na wahadhiri waweze kuimudu ipasavyo sio tu taaluma hii, bali taaluma zingine za kiisimu ambazo hazina marejeleo ya kutosha yaliyotafsiriwa.

Vitabu vingi vya kiada hasa vya kinadharia bado vipo katika lugha za kigeni. Mfumko wa istilahi mbalimbali za kifasihi zinazoibuka kila uchao miongoni mwa waandishi na wahakiki wa fasihi ya Kiswahili unahitaji kupitia katika usanifishaji ili kazi ya kutafsiri iwe na uwiano mzuri. Hivi sasa kuna shehena kubwa ya istilahi ghafi ambazo zinatumiwa kiholela tu na wafasiri mbalimbali. Hili linaweza kumtatiza msomaji wa matini za kifasihi zilizotafsiriwa. Ipo haja kwa serikali za nchi za Afrika Mashariki kuharakisha uasisi wa Tume ya Kiswahili ya Afrika Mashariki ili taasisi hii iweze kuratibu na kurahisisha matumizi ya Kiswahili pamoja na shughuli za utafsiri kwa lengo la kuiendeleza lugha hii ulimwenguni. Kupitia vyombo vya kukuza Kiswahili kama vile Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI), Chama cha Kiswahili cha Taifa Kenya (CHAKITA), Chama cha Kiswahili Afrika Mashariki (CHAKAMA) na vinginevyo, wasomi wa Kiswahili wanaweza kuunda majopo ya tafsiri ili kuhimiza kutafsiriwa kwa tanzu mbalimbali za fasihi za kiasili, hususan katika eneo la Afrika Mashariki kwa lugha ya Kiswahili. Hii itasaidia kuzihifadhi kwa vizazi vijavyo. Tafsiri hizi zinaweza pia kufanywa kwa lugha zilizoko nje ya eneo hili, hasa zile za kimagharibi, ili kuzijumuisha pamoja na fasihi za kimataifa zilizoko. Wafasiri wa Kiswahili walio na weledi wa lugha za kigeni wanaweza pia kuchukua jukumu la kutafsiri kazi za fasihi ya Kiswahili zilizoko ili ziweze kujulikana nje ya mipaka ya nchi hizi. Mazao haya ya kifasihi yataenea kwa haraka kutokana na kasi iliyoko ya mawasiliano ya kiteknolojia. Hii itasaidia kusambaza fasihi za nchi hizi kwa mataifa ya ulimwengu. Aidha, ushirikiano baina ya wataalamu wa Kiswahili waliobobea katika taaluma ya tafsiri na wataalamu wa filamu wanaweza kuzalisha filamu za vibonzo kwa lugha ya Kiswahili kwa kutumia fasihi za kiasili, hususan hadithi na masimulizi ya jadi. Kwa kutumia mtandao wa mawasiliano, filamu hizi zinaweza kusambazwa ulimwenguni ili kukuza sio tu lugha hii bali pia fasihi na utamaduni wa eneo la Afrika Mashariki. Mwisho, bali si akali, vyuo vikuu Afrika Mashariki vinahitaji kutayarisha mitalaa mahususi ya kufunza taaluma za ukalimani na tafsiri, hususan kwa kutumia njia za kiteknolojia ili ufasiri uwe mchakato endelevu wa kuziwezesha fasihi za Afrika Mashariki kuwa za kimataifa.

**Marejeo**

Aiello, F.T (2005), "Translating a Swahili Novel into 'Kizungu'". *Swahili Forum 12. pgs. 99-107*

Catford, J.C (1974), *A Linguistic Theory of Translation*, London: Oxford University Press

Kelly, L.G (1979), *The True Interpreter: A History of Translation, Theory and Practice In the West*, Bristol: Basil Blackwell

Knappert, J (1979), *Four Centuries of Swahili Verse*, London: Leiden

Masoko, D.LW (2006), "Tafsiri ya Riwaya ya Bw. Myombekere na Bibi Bugonoka Ntulanalwo na Bulihwali: Juzuu I&II" katika *Kitangulizi cha Tafsiri*, TUKI: Dar es salaam. kur.71-84

Mtesigwa, P.C.K (2006) "Kitabu cha Wimbo wa Lawino kama Tafsiri ya Ushairi" katika *Kitangulizi cha Tafsiri*, TUKI: Dar es Salaam. kur.88-99

Mwansoko, H.J.M (2006) "Dhana, Dhima na Historia ya Tafsiri" katika *Kitangulizi cha Tafsiri*, TUKI: Dar es Salaam

Newmark, P (1988), *Approaches to Translation*, London: Prentice Hall International (UK) Ltd

Omboga, Z (1986), "Fasihi Tafsiri katika Ukuzaji wa Fasihi ya Kiswahili: Matatizo na Athari zake" Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi

Snell-Hornby, M (2006), *The Turns of translation Studies: New Paradigms or Shifting Viewpoints?* John Benjamin Publishing Company

Temu, C.W (1972), "Swahili Vocabulary Expansion: A Preliminary Observation"katika *KISWAHILI Vol. 42/1 Machi 1972*, TUKI: Dar es Salaam

Zhukov, A (1998) "Shaaban Robert in the Russian Language". *Swahili Forum 5. Pgs. 185-189*